

Vita ya kugombania maji inavyoinyemelea dunia

Na Albano Midelo



Matumizi ya maji duniani yameongezeka mara sita zaidi kati ya mwaka 1900 na 1995 zaidi ya mara mbili ya kiwango cha ongezeko la watu na huendelea kukua kadiri kilimo viwanda na matumizi ya nyumbani yanavyoongezeka. Kilimo hutumia takribani asilimia 70 ya matumizi yote ya maji duniani.

Nchi ya Somalia inakabiliwa na ukame wa kutisha ambapo watu milioni sita kati ya milioni kumi wapo katika vita ya kugombania maji na chakula baada ya vyanzo vingi vya maji kukauka na kusababisha njaa katika maeneo mbalimbali ya nchi hiyo.

Maelfu ya watu wanayahama makazi yao nchini Somalia katika harakati za kutafuta maji, chakula na maeneo ya malisho ya mifugo yao, hiyo ikiwa ishara ya kiwango cha mzozo wa maji na chakula unaolikumba taifa hilo.

Mwandishi Jacob Safari wa Shirika la Save The Children anasema kuwa Serikali za mikoa na maafisa wa shirika la kuwasaidia watoto la Save the

Children wanaripoti kwamba mamia ya malori yaliyosheheni familia na mifugo yamekuwa yakiwasili katika maeneo ya pwani ya Puntland katika kipindi cha wiki sita zilizopita na yamekuwa yakiwapeleka katika maeneo ya mbali kama Somaliland, kwa kuwa walisikia kwamba kulinyesha mvua kabla sikukuu ya Krismasi mwaka uliopita.

Katika eneo la kati upande wa kusini mwa Somalia, Umoja wa Mataifa unaripoti kwamba zaidi ya wakimbizi 100, wasomali waliokabiliwa na ukame wamekuwa wakivuka mpaka wa Ethiopia na kuingia kambi ya Dollo Ado tangu Januari 2017, jambo ambalo halijaonekana katika miaka minne.

Huko Puntland, eneo linalokabiliwa na ukame mbaya zaidi tangu mwaka wa 1950, wakimbizi wapya wa ndani waliopoteza mifugo yao wanakusanyika katika kambi zisizo rasmi wakitafuta maji, chakula na misaada. Ingawa familia zinapata wakati mgumu kukabiliana na hali hiyo kutokana na bei za juu za maji na chakula.

"Hali ya ukame imekuwa mbaya na haijawahi kuwa hivi kwa miongo kadhaa na mizoga ya mbuzi imezagaa kila mahali," anasema Hassan Noor Saadi Mkurugenzi wa Shirika la Save the Children nchi Somalia.



Kutokana na hali hiyo Umoja wa Mataifa ulitoa tahadhari ya kutokea ukame wa kutisha katika nchi ya Somalia huku zaidi ya watu milioni sita wanakabiliwa na tatizo la usalama wa upatikanaji wa maji na chakula.

Ukame umetokana na uhaba wa mvua ambao umesababisha vyanzo vingi vya maji kukauka ambapo watoto 71,000 tayari wanakumbwa na utopia mlo na wako katika hatari ya kufa, huku zaidi ya watoto 360,000 walio chini ya miaka mitano wakikabiliwa na tatizo hilo kulingana na Shirika la Save the Children.

Kwa mujibu wa wa Umoja wa Mataifa, Somalia imeshuhudia misimu ya kufuatana ya uhaba wa mvua, hii ikiwa na maana kwamba ukame tayari umeharibu mimea na kuuwa mifugo katika maeneo yaliyoathirika zaidi. Ukame huu wa sasa umeyaathiri mataifa jirani ya Kenya na Ethiopia.

Nchi hiyo imeingia katika vita ya kugombania maji na chakula na kuleta hali mbaya zaidi ya ukame iwapo hakutatolewa fedha za misaada, maji na dawa ili ziwafikie wale walioathirika zaidi hususan watoto. Ukame nchini Somalia kati ya mwaka 2010 na 2012 ulikadiriwa kuwauwa watu kati ya 260,000, wengi wao ni watoto.

Shirika la Afya Duniani WHO linasema zaidi ya watu milioni tano hufa kutokana magonjwa yatokanayo na maji kila mwaka ambayo ni mara kumi ya idadi ya watu wanaokufa kutokana na vita. Mamilioni ya watu duniani hutegemea maji ili waishi, na kukosekana kwake husababisha vifo .

Kwa mujibu wa WHO, watu bilioni 1.3 ambao ni moja ya tano ya watu wote duniani wanakosa maji salama ya kunywa, na asilimia 40 ya watu wanakosa huduma za kimsingi za afya. Mwenyekiti wa Baraza la Maji Duniani Loic Fauchon anakiri hivi sasa hali ya upatikanaji wa maji duniani ni mbaya na kwamba watu wengi wanaweza kuangamia kwa kukosa maji safi na salama kutokana na uchafuzi wa vyanzo vya maji unaoendelea duniani kote.

"Leo tunajadili suala la maji ambalo linawatia watu wasiwasi, na linaweza kusababisha migogoro na vita vya maji vya Dunia. Hivi sasa rasilimali ya maji ipo hatarini kutoweka, binadamu wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji. Watu waliokufa mwaka 2014 kutokana na uchafuzi wa maji, ni mara 10 ya waliokufa kutokana na vita. Kila asubuhi mamilioni ya wanawake na watoto wanateka maji kiasi kidogo tu yasiyo safi kwa kusafiri kwa miguu kwa saa kadhaa." Anasema Fauchon.

Jumuiya ya Kimataifa imefanya juhudi kubwa ili kutatua suala la upungufu wa maji. Kwa mujibu wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa yaliyopitishwa kwenye Mkutano wa viongozi wa Milenia wa Umoja wa Mataifa uliofanyika mwaka 2000 huko New York nchini Marekani, idadi ya watu wanaokosa maji salama ya kunywa ilitakiwa kupungua kwa nusu kabla ya mwaka 2015.

Mipango ya utekelezaji wa kutatua upungufu wa maji duniani kuanzia mwaka 2005 hadi 2015 ilipitishwa kwenye Mkutano wa viongozi wa dunia uliofanyika mwaka 2002 huko Johannesburg, Afrika ya Kusini.

Katika mkutano huo ilipangwa miaka 10 ya utekelezaji mpango wa "Maji ni Uhai" wa Umoja wa Mataifa ambapo Rais Vicente Fox wa Mexico anasema, serikali zote zinapaswa kutatua suala la maji kwa hatua zenye ufanisi, jambo ambalo limeshindikana kwa kuwa tatizo la maji linaendelea kuongezeka na kuiacha Dunia njia panda.

Katika ripoti hiyo ya WaterAid imeonesha kuwa kuna watu zaidi ya milioni 660 duniani kote wanakosa maji safi na salama na wengi wao wakiwa ni watu ambao wanaishi maeneo ya vijijini.

"Kwa sasa kuna watu milioni 663 duniani kote ambao wanakosa maji safi na wengi wao wanaofikia milioni 552 wanaishi maeneo ya vijijini," imesema ripoti ya WaterAid.

Aidha imezitaja nchi ambazo zina hali mbaya zaidi kuwa ni Papua New Guinea, Mozambique and Madagascar na Angola ambayo inangoza ikiwa na asilimia 71 ya wananchi wake wa vijijini wakikosa maji safi na salama.

Pia ripoti ya WaterAid imesema kuwa asilimia 20 ya mataifa yote duniani yameshapata athari kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Kwa mujibu wa Shirika la Water Aid, asilimia 56 tu ya watanzania milioni 52 wenye uwezo wa kupata maji toka vyanzo salama ambapo zaidi ya watanzania milioni 23 wanakunywa maji kutoka katika vyanzo visivyo salama.

Takwimu zinaonesha kuwa watoto 3000 waliopo chini ya miaka mitano, wanakufa kila mwaka kutokana na magonjwa ya kuhara yanayoweza kuzuilika yanayotokana na matumizi ya maji siokuwa safi na salama, pamoja na matumizi ya vyoo siokuwa sahihi.

Asilimia 60 ya Tanzania ni jangwa



Tatizo ukataji wa miti na misitu hovy limesababisha nchi yetu kuwa na zaidi ya asilimia 60 ya eneo lililoathiriwa na jangwa kwa kuwa vyanzo vingi vya maji vimeendelea kukauka mwaka hadi mwaka. Takwimu zinaonesha kuwa nchi yetu kila baada ya wastani wa miaka minne kunatokea ukame na kuathiri karibu watu milioni 3.6 katika Sehemu za Dodoma, Singida, Shinyanga, Mwanza na Mara.

kutokana na ukataji wa misitu, kilimo kisicho cha kitaalam kumesababisha mmomonyoko wa ardhi na kusababisha udongo kupoteza rutuba na hivyo kusababisha ukosefu wa mvua na mafuriko ambayo huwaathiri wananchi kila mwaka.

Uharibifu wa mazingira nchini sio unaleta athari katika ardhi na maji tu lakini pia unachafua hewa na kusababisha madhara makubwa kwa afya ya wanadamu na viumbe vingine hai ambavyo hutegemea hewa safi ili viweze kuendelea kuishi.

Hali halisi inayoendelea hivi sasa inathibitisha kuwa taasisi zinazoshughulikia mazingira zimeshindwa kuzuia uharibifu wa mazingira licha ya kuwepo sera na sheria matokeo yake watanzania wengi wanapata athari za kiafya na kimazingira hali hii ni mbaya kwa kuwa siku moja tunaweza kuangamia sote.

Kutokana na uchafuzi huo wa mazingira historia inaonesha kutoka mwaka 1980 hadi 2015 mafuriko nchini mwetu yameshatokea mara nyingi na kusababisha vifo vya watu na wengine kuathiriwa vibaya katika makazi yao hasa katika Sehemu za Tanga, Dar es salaam, Mbeya, Zanzibar, pemba, Geita, Shinyanga, Pwani, Morogoro, Arusha, Rukwa, Iringa, Kigoma, Lindi na Dodoma.

Sheria zipo kinachotakiwa ni kuhakikisha sheria hizo zinachukua nafasi yake kwa wale wote watakaobainika kwenda kinyume na sheria za mazingira ukiwemo ukataji wa misitu na uchafuzi wa vyanzo vya maji. Tusipoangalia vita kuu ya tatu ya Dunia inakuja tutaangamia sote.

Mwandishi anapatikana kwa baruapepe: albano.midelo@gmail.com, simu 0784765917